

WIZARA YA ELIMU SAYANSI,TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI.

SHULE YA SEKONDARI YA MANDA.  
S.L.P.7,  
LUDEWA,

01/12/2020.

Kumb.Na.makoss/join/vol./3/020

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH.MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MANDA, WILAYA YA LUDEWA ,Mkoa wa NJOMBE MWAKA, 2021.

### 1.0.UTANGULIZI.

Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.Shule ya sekondari manda ipo mwambao mwa ziwa nyasa ,kata ya manda , tarafa ya masasi,wilaya ya ludewa.

Muhula wa kuanza wa masomo utanza tarehe 11/01/2021.Unatakiwa kuripotishuleni kuanzia tarehe 11/01/2021.Na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2021.

### 2.0.MAMBO YA KUZINGATIA

#### A.SARE ZA SHULE

WAVULANA ni suruali moja ya khaki na tai yake na suruali moja nyeusi ya tetroni na tai yake.shati mbili nyeupe mikono mirefu ya tetron .viatu vya ngozi kisigino kifupi,vya kufunga kamba pea mbili, soksi nyeusi pea mbili.suruali iwe pana na isiwe modo lazima iwe na selesheni mbili au tatu.Tisheti rangi ya kijani yenye nembo ya shule,itapatikana shuleni kwa tshs.10,000/=

WASICHANA ni visolo viwili vyeupe vya tetron mikono mifupi, aje na suruali moja ya khaki na suruali ya pili nyeusi ziwe pana na zisiwe modo .viatu vya ngozi vyeusi vya kamba pea 2 .na viwe na visigino vifupi ,aje na soksi nyeupe pea 2.Tisheti rangi ya kijani yenye nembo ya shule itapatikana shuleni kwa SHS.10,000/=

#### B)SARE ZA MICHEZO

WAVULANA: Tracksuit rangi ya blue yenye pundamilia nyeupe, ziwe mbili na raba nyeusi .bukta rangi ya blue bahari pea mbili

WASICHANA: Tracksuit rangi ya darkblue yenye pundamilia nyeupe na,raba nyeusi,bukta pens nyanya rangi nyeusi.Aje na sketi 1 ya khaki na nyingine 1 nyeusi kwa ajili kuvalia nje ya suluali wakati wa kazi za nje.

### **C)VIFAA MUHIMU VYA DARASANI**

- i) Daftari kubwa counterbooks quire 2, ziwe 12 na peni 8 za kunzia.
- ii) Mkebe na vifaa vyake ndani
- iii) Rula ndogo moja penseli aina ya HB na mfuto wake, na kichonge.
- iv) Mkoba wa kubebea daftari. Isiwe kifungashio
- v) Daftari ndogo 10,za kufanyia mitihani ya kila wiki.

### **D)CHAKULA CHA MCHANA SHULENI**

Kamati ya chakula ya wazazi , itatoa chakula cha mchana shuleni,hivyo mwanao aje na michango muhimu ifutayo:

#### **I.WANAFUNZI WANAOTAKAO KAA HOSTER.**

- 1.MAHINNDI , MADEBE 6 KWA MWAKA ,NUSU MWAKA DEBE 3.
- 2.MAHARAGE ,MADEBE 2 KWA MWAKA ,NUSU MWAKA DEBE 1.
- 3.FEDHA TASLIM TSHS.51,000/= KWA MWAKA,(Kwa ajili ya wapishi,kusaga,na viungo.NUSU MWAKA TSHS.25,500/=

#### **II.WANAFUNZI WA KUTWA**

- 1.MAHINDI MADEBE 4 KWA MWAKA,NUSU MWAKA MADEBE 2
- 2.MAHARAGE DEBE 1 KWA MWAKA,NUSU MWAKA LITA10.
- 3.FEDHA TASLIMU ...TSHS.51000/=,NUSU MWAKA TSHS 25,500/=

#### **III.VIFAA MUHIMU KWA WANAFUNZI WA HOSTERI.**

- I. Shuka mbili ,rangi ya pink
- II. Blanket moja,
- III. Ndoo za lita 10, mbili,moja ya kuogea na y a pili ya kuchotea maji ya kupikia.
- IV. Jembe 1 na kwanja 1 au panga kwa ajili ya usafi wa mazingira shuleni.
- V. Container ya kulia chakula 1,kijiko na kikombe cha kunywea uji 1.
- VI. Bima ya Afya ni muhimu sana.Aje nayo shuleni,
- VII. Vifaa vya usafi binafsi,Sabuni za kufulia nakuogea,mafuta ya kupakaa,mswaki na dawa ya meno ,whit dent.n.k.

#### **IV.VIFAA MUHIMU KWA WANAFUNZI WA KUTWA**

- I .Ndoo ya kuchotea maji ya lita 10 ,moja.
- II .Jembe 1 na kwanja 1 au panga 1 kwa ajili ya usafi wa mazingira shuleni.
- III.Container ya kulia chakula 1,kijiko na kikombe cha kunywea uji 1.
- IV.Bima ya Afya ni muhimu sana.

### 3.0.SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka1978 na marekebisho yake kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha ,inazingatia miongozo inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi na ofisi ya waziri mkuu-TAMISEMI,yenye jukumu la usimamizi na uendashaji wa elimu nchini.

#### 3.1.KANUNI ZA SHULE

- 1.Heshima kwa viongozi ,wazazi, wafanyakazi, wanafunzi na jamii yote
- 2.Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya darasa.kulinnga na ratiba ya shulea
- 3.kushiriki kwa makini maandario ya jioni(preparation)
- 4.kuwahi kwenye kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.
- 5.kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo ya juu kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote.
- 6.kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- 7.kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- 8.kuzingatia ratiba ya shule ,wakati wote.
- 9.kutunza mali ya umma.

#### 3.2.SHERIA ZA SHULE

#### MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- 1) .wizi
  - 2) Uasherati
  - 3) Ubakaji
  - 4) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
  - 5) Kupiga au kupigana
  - 6) Kuharibu kwa makusudi mali y umma
  - 7) Kudharau bendera ya taifa
  - 8) Kupata mimba
  - 9) Kuo au kuolewa
  - 10) kutoa mimba
  - 11) kugoma au kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama washule au watu
  - 12) kukataa adhabu kwa makusudi.
- 4.0.Tafadhari soma kwa makini maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

.....  
**Mgaya R.L,**

***MKUU WASHULE***